**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**S. L. P. 08,**
**KIOMBOI – IRAMBA - SINGIDA,**

**NAMBA ZA SIMU:**
**MKUU WA SHULE: 0787439490/0769655851**
**E-mail: lulumbass1991@gmail.com**

**MZAZI WA MWANAFUNZI**
**…………………………………………….**
**S.L.P. ………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LULUMBA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA MKOA WA SINGIDA MWAKA 2022.**

**1.0.UTANGULIZI**

Napenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari LULUMBA, Hongera sana. Hii imetokana na bidii na juhudi zako ulizozionesha katika masomo yako ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

Shule ya sekondari LULUMBA ni shule yenye wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita, ni shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne (wasichana na wavulana). Vilevile ni shule ya bweni kwa kidato cha tano na sita (Wavulana). Tunakukaribisha sana ili upate elimu bora.

Aidha nafasi uliyoipata ni ya kujivunia na unatakiwa kuitumia vema kwa manufaa yako, familia na taifa kwa ujumla. Kumbuka, '**Elimu ni Ufunguo wa Maisha'** itafute kwa bidii. Kiwango cha ubora wa maisha ya usoni kwa kila mtanzania na taifa kinategemea maandalizi yako ya sasa katika elimu bora ili kuikwamua jamii hususani familia yako inayowekeza katika **ELIMU BORA NA ENDELEVU** katika janga la ujinga na umasikini.

1.1 **KAULI MBIU, DIRA, DHAMIRA NA WIMBO WA SHULE**

**1:1.1 KAULI MBIU (MOTTO)**

- Kauli mbiu ya shule ni elimu hushinda vyote *"EDUCATION CONQUERS ALL "*

**1:1.2 DIRA (VISION)**

- Dira ya shule yetu ni – kutoa elimu bora ili kuendeleza jamii yetu

*"PROVISION OF QUALITY EDUCATION IN ORDER TO DEVELOP OUR SOCIETY"*

**1:1.3 DHAMIRA (MISSION)**

- Dhamira ya shule hii ni kuwa, kila mwanafunzi lazima apate elimu bora

*"EVERY STUDENT SHOULD ACHIEVE QUALITY EDUCATION"*

**1:1. 4 WIMBO WA SHULE.**

- Lulumba sekondari inao wimbo ambao kila mwanafunzi anapaswa aufahamu.
- Yafuatayo ni maneno ya wimbo huo.

1. *Lulumba yetu shule ya sekondari, ninaipenda kwa moyo wangu wote.*
   *Mandhari yake yanavutia sana, elimu pia motomoto.*

Chorus Elimu ndiyo motto wa shule yetu, Nidhamu ndiyo ngao yetu, muungano pamoja na mashauri, utu, umoja na upendo.

2. Shule yetu ina walimu wazuri, wenye ujuzi mwingi wa kufundisha, wanafunzi pia tunawajibika, masomo ndio ngao yetu.

3. Shule iliko ni Wilaya Iramba, mashariki mwa mji wa Misigirii, imepambwa kwa miti nayo maua, ukipita utaiona.

## 2.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA

- Shule ni ya mchepuo wa sayansi tu kwa michepuo ya **PCM, PCB** na **CBG**. Hivyo, masomo yanayofundishwa ni pamoja na Physics, Chemistry, Biology, Advanced mathematics, Basic applied mathematics, Geography na General studies.

## 3.0 MAHALI SHULE ILIPO

- Shule ipo katika makao makuu ya Wilaya ya Iramba (Kiomboi) Mkoa wa Singida Ukifika MISIGIRI kutokea Nzega au Singida mjini utapata usafiri wa moja kwa moja hadi Kiomboi, Pia kuna magari ya moja kwa moja kutoka Dar es salaam, Arusha na Kilimanjaro mpaka Kiomboi ambayo ni makampuni ya usafirishaji ya JMC EXPRESS, ESTHER LUXURY COACH (DSM TO KIOMBOI) na KANDAHARI INV. LTD (KILIMANJARO, ARUSHA TO KIOMBOI). Kwa wanaosafiri kutokea mikoa ya Kanda ya ziwa, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Katavi na Tabora, washukie njia panda ya MISIGIRI na wapande magari yanayoelekea Mji wa Kiomboi na washukie kituo cha shule ya sekondari LULUMBA.

## 4.0 KUFUNGUA SHULE

- Shule itafunguliwa **mara tu serikali itakapotoa tamko na maelekezo mengine ya ufunguzi wa shule** na unatakiwa kuripoti siku itakayoelekezwa na serikali. (Kama utapata udhuru wa kutokufika siku hiyo, wasiliana kwa namba za simu zilizopo hapo juu).

## 4.1 OFISI UTAKAZOPOKELEWA

- Ukifika shuleni nenda moja kwa moja **ofisi ya mkuu wa shule** kwaajili ya maelekezo na utaratibu za usajili.
- Muda wa usajili ni kuanzia saa **1:30 Asubuhi** hadi **saa 12:00 Jioni**.

**5.0 MAHITAJI YA SHULE**

**5.1 ADA NA MICHANGO YA SHULE**

| S/N | AINA YA MCHANGO | MUHULA WA KWANZA | MUHULA WA PILI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| i) | Ada | Tshs. 35,000/= | Tshs. 35,000/= | Tshs. 70,000/= |
| ii) | Taaluma | Tshs. 15,000/= | Tshs. 15,000/= | Tshs. 30,000/= |
| iii) | Fedha ya tahadhari (haitarejeshwa) | Tshs. 5,000/= | ---- | Tshs. 5,000/= |
| iv) | Mchango wa mlinzi | Tshs. 10,000/= | ---- | Tshs. 10,000/= |
| v) | Mchango wa dawati | Tshs. 15,000/= | ---- | Tshs. 15,000/= |
| vi) | Mchango wa wapishi | Tshs. 10,000/= | Tshs. 10,000/= | Tshs. 20,000/= |
| vii) | Mchango wa ukarabati | Tshs. 15,000/= | Tshs. 15,000/= | Tshs. 30,000/= |
| viii) | Mchango wa kitambulisho na picha | Tshs. 6,000/= | ---- | Tshs. 6,000/= |
| ix) | Mchango wa nembo ya shule | Tshs. 2,000/= | ---- | Tshs. 2,000/= |
| **JUMLA** | | **Tshs. 113,000/=** | **Tshs. 75,000/=** | **Tshs. 188,000/=** |

**NB.**

- Kama mwanafunzi ana bima ya afya (NHIF) aje nayo wakati wa kuripoti ili awe anaitumia katika matibabu na kama hana bima ya afya (NHIF) aje na shilingi elfu sita (Tshs. 6,000/=) na atapewa maelekezo ya namna ya kuipata huduma ya bima ya afya (CHF).
- Fedha ya michango ya shule italipwa kwenye:

JINA LA ACCOUNT: ***LULUMBA SECONDARY SCHOOL CAPITATION GRANT.***
ACCOUNT NAMBA: ***50601100137.***
JINA LA BENKI: ***NMB.***

- **Tafadhali unapofanya malipo andika jina la mwanafunzi husika anayelipiwa mchango (michango) kwenye Bank Pay in Slip na si vinginevyo.**
- Mwanafunzi atakayekuja bila kulipa michango iliyoainishwa kwenye jedwali juu **HATAPOKELEWA** .

**5.2 MAHITAJI YA TAALUMA**

i. Rimu mbili (1) A-4 aina ya **PAPERONE (Copier)** na siyo aina nyingine. (rimu moja (1) italetwa mwanafunzi anaporipoti shuleni
ii. Jalada au file jipya lenye kamba kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi.
iii. Scientific calculator – function 991.
iv. Madaftari yanayotosheleza matumizi ya mwanafunzi kwa mwaka mzima
v. Vitabu vinavyoendana na tahasusi (Combination) ya mwanafunzi. Unashauriwa kuja na vitabu angalau viwili kwa kila somo kulingana na tahasusi unayosoma. Yafuatayo ni mapendekezo ya aina za vitabu vinavyotumika kwa kidato cha tano na sita:

| SOMO | BIOLOGY | PHYSICS | CHEMISTRY | ADVANCED MATHEMATICS | GEOGRAPHY | GENERAL STUDIES | BASIC APPLIED MATHEMATICS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **AINA YA VITABU** | -Biologica Science.<br>-Comprehensive Biology.<br>-Understanding Biology.<br>-CHAND. | -Principles of Physics by Nelkon 5th Ed.<br>-CHAND Class XI and XII.<br>-ABC Modern Physics 1,2.<br>-Roger Muncaster. | - CHAND XI and XII.<br>-A-Level Chemistry Ramsden 4th Ed.<br>-Conceptual Chemistry.<br>-Organic Chemistry Part I & II.<br>-Inorganic Chemistry Part I & II.<br>-Soil Chemistry.<br>-Physical Chemistry for A-Level. | -CHAND Class XI & XII<br>-Pure Mathematics I & II by Back House.<br>-Advanced Mathematics by Tranter. | -Unintegrated Regional Study on Human and Economic Geography by D.T. Msabila.<br>-Physical Geographyin Diagram by Bunnett. | -Nyangwine N. et al (2012) CONTEMPORARY APPROACH FOR ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES NOTES FORM 5 & 6.<br>-UNDERSTANDING ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES (ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL EDUCATION) BY Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratias | -Applied Mathematics by CHAND S.<br>-A text Book of Applied Mathematics by Dr. J.S. Bindra. |

**5.3 MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI, MALAZI NA CHAKULA**

i. Mfagio wa sakafu mmoja (soft bloom) kwa michepuo yote.
ii. Jembe moja (1) lenye mpini kwa mchepuo wa PCB.
iii. Fyekeo (kwanja) moja (1) kwa mchepuo wa PCM
iv. Fyekeo (kwanja) moja (1) kwa mchepuo wa CBG.
v. Godoro moja (1) (ft 2.5x6)
vi. Shuka mbili (2) rangi ya light blue na folonya rangi ya light blue
vii. Chandarua kimoja (1)
viii. Blanket moja .
ix. Vyombo vya chakula :- kijiko, kikombe, bakuli na sahani.
x. Ndoo mbili (2) ndogo zenye mifuniko na galoni ya kutunzia maji ya kunywa.

**Angalizo:** Mafuta ya kubadilisha rangi ya ngozi, mafuta yenye harufu kali (perfume, body spray) **HAZIRUHUSIWI**

**5.4 SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORMS)**

**5.4.1. Sare ya Shule.**

i. Mwanafunzi anapaswa kuja na suruali mbili (2) za bluu bahari zenye marinda mawili ya cross pembeni, mfuko mmoja wa nyuma upande wa kulia na upana chini ya miguu uwe inchi 17 (isiwe modo),
ii. Tai mbili (2) rangi ya bluu bahari,
iii. Shati mbili (2) **TETRON** za rangi nyeupe za mikono mirefu ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja tu kushoto (Zitavaliwa kwa kuchomekewa),
iv. Sweta moja (1) rangi ya bluu bahari na
v. T-shirt moja (1) nzito ya njano yenye kola isiyokuwa na maandishi yoyote.
vi. Viatu vya ngozi rangi nyeusi vinavyofunika miguu vyenye kamba na kisigino kifupi (boot na raba nyeusi haziruhusiwi)
vii. Jozi mbili za soksi nyeusi zisizo na mapambo wala maandishi yoyote.
viii. Mkanda **mweusi wa ngozi** wa kuvalia suruali.

**5.4.2**. **Sare ya Michezo.**

i. Jezi (bukta na Tshirt yenye rangi ya Taifa Stars na viatu vya michezo.
ii. Tracker ya rangi ya blue bahari**,**

**5.4.3**. **Shamba Dress.**

i. T-shirt ya rangi ya dark blue aina ya form six isiyokuwa na maandishi yoyote.
ii. Suruali nyeusi yenye marinda mawili ya cross pembeni, mfuko mmoja wa nyuma upande wa kulia na upana chini ya miguu uwe inchi 17 (isiwe modo),
**KUMBUKA:** Sampuli za Picha za mionekano ya sare za shule zimeoneshwa katika fomu hii. **Tafadhali zingatia mionekano ya rangi zilizoainishwa.**

**6.0 TAALUMA.**

- Shule hii inajali sana taaluma bora kwa wanafunzi wote. Hivyo mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga Lulumba Sekondari ana bahati na atatakiwa kusoma kwa bidii zote na kuachana na tabia zitakazomuathiri kimasomo ili aweze kufaulu vizuri masomo yake. Shule haitawavumilia kabisa wanafunzi wanaotoroka darasani. Utaratibu wa wiki nzima (school routine ) utatolewa na kumpa fursa mwanafunzi kufuata kwa ukamilifu ratiba ya shule. Aidha kutokufanya mtihani au jaribio ni kosa linaloweza kumsababishia mwanafunzi kupoteza nafasi yake ya kuwa shuleni .

**7.0 HESHIMA, ADABU, UTII**

**7.1 HESHIMA, ADABU, UTII**

Mwanafunzi aliyepata nafasi ya kujiunga na shule hii hana budi kuwa na adabu, utii na heshima kwa walimu wake, watumishi wengine, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla. Mwanafunzi atakayebainika kutokuwa na tabia njema, au kuwa jeuri **ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA**. Aidha mzazi anatakiwa amwonye mwanae na kumtahadharisha na tabia za kutofuata sheria za shule.

**7.2 SHERIA ZA SHULE**

Sheria zifuatazo zinatakiwa kuzingatiwa na mwanafunzi siku zote awapo shuleni na mahali pengine popote nje ya shule:

1. Mwanafunzi lazima awe na utii na hekima kwa walimu, viongozi, watu wazima, wageni na kati yao wenyewe.
2. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mali za shule.
3. Wanafunzi hawaruhusiwi kuvuta sigara, kunywa pombe, kunywa vidonge vya kulevya au kuvuta bangi na wizi.
4. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu bila ruhusa au nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
5. Ni marufuku kuingia nyumba za starehe kama vile bar, dansini (ukumbi wa disco) na nyumba za kulala wageni (guest houses).
6. Ni wajibu wa wanafunzi kuona kuwa viwanja vya shule, madarasa na vyumba vingine vimewekwa katika hali ya usafi.
7. Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi ni marufuku.
8. Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vya dini yake kila siku.
9. Ni mwiko kwa wanafunzi kujiunga na vikundi vyenye tabia mbaya shuleni au nje ya shule.
10. Kila mwanafunzi anapaswa kuhwahi shuleni saa 6.30 asubuhi kwa ajili ya kuhesabu namba na kuendelea na ratiba ya shule kama ilivyoainishwa na utawala.
11. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu katika mipango yote ya shule ya elimu ya kujitegemea. Uvivu au utoro ni makosa makubwa.
12. Ni marufuku kupokea wageni. Wageni wote wapiti kwa mkuu wa shule.
13. Ni marufuku kuzagaa nje ya madarsa wakati wa vipindi.
14. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia au kuchemsha chochote awapo shuleni ispokuwa kwa ruhusa maalumu kutoka utawala.
15. Ni marufuku kujiunganishia au kuunganisha umeme katika maeneo yoyote ya shule.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo au viatu ambavyo siyo sare ya shule ndani nan je ya shule.
17. Ni marufuku kuonekana ama kulala bwenini wakati vipindi vinaendelea darasani au wakati wa maandalizi ya usiku “NIGHT PREPARATION”
18. Simu za mkononi haziruhusiwi kabisa shuleni; mwanafunzi akikamatwa na simu shuleni atafukuzwa shule mara moja.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kugomea adhabu.
20. Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti shuleni akitokea likizo. Endapo atafanya hivyo, atarudishwa nyumbani kumfuata mzazi wake ili aeleze sababu za kuchelewa kufika shule kwa wakati. Kama sababu za mzazi hazitajitoshereza, mwanafunzi atapewa adhabu stahiki kwa kuzingatia maoni ya ofisi ya nidhamu.

- **MAKOSA MENGINE YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE NI PAMOJA NA:-**

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
4. Kupigana au kupiga.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
6. Kudharau bendera ya taifa.
7. Kuoa au kuolewa.
8. Kusababisha mimba au kushiriki kutoa mimba.
9. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

**8.0 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU.**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali yoyote ya serikali.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi – mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
v. Picha za mfano zikionesha sare za shule kulingangana na maelekezo yaliyotolewa katika kipengele cha **SARE YA SHULE.**

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo – maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**




**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI LULUMB**

MKUU WA SHULE
LULUMBA SEKONDARI
S.L.P. 08
KIOMBOI-SINGIDA

..............................................................

**YEREMIA M. KITIKU**
**MKUU WA SHULE**

**PRESIDENT’S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

LULUMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 08,
KIOMBOI,
DATE…………………………..

To the medical officer,
……………………………………………………………..
Dear Sir/Madam

**REF: <u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION</u>:-**

Please examine Mr/Miss …………………………………………………………………………… As to his/her fitness as a full time (student of this school) may I kindly requests you to fill in the particulars given in the form here under.
(Yours Sincerely).
…………………………………………………………
The Headmaster
……………………………………………………………

<u>TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER</u>

1. Blood count (White blood cells)……………………………………………….
2. Stool examination……………………………………………………………
3. Urine examination……………………………………………………………
4. Gestation (for girls only)…………………………………………………….
5. Venereal diseases…………………………………………………………….
6. T.B test…………………………………………………………………………
7. E.N.T problem………………………………………………………………….
8. Defects of (a) The left and right eye………………………………………..
   (b) The Chest…………………………………………………
9. Does he/she has any CHRONIC disease eg. Epilepsy cell, Anemia, Athma etc.

…………………………………………………………………………………………………
…..........................................................................................................................................

I have examined Mr/Miss ………………………………………………. And certify that he/she is physically fit to persue studies as stated above

………………………………………………………………………………………
Name and Signature of the medical officer

Date……………………………………
Designation…………………………..

**FOMU NA PICHA ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA NAMBA ZAO ZA SIMU.**

| NA | JINA LA NDUGU | MAHUSIANO | NAMBA YA SIMU | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ………………………………. | …………………. | ………………… | |
| 2 | ………………………………. | …………………. | ………………… | |
| 3 | ……………………………….. | ………………….. | ………………… | |
| 4 | ……………………………… | …………………... | ………………… | |

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAYOTOLEWA NA SHULE.**

Mimi…………………………………………………. (jina la mwanafunzi) nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na maagizo yote yanayoelekezwa katika barua ya maelezo niliyopewa na shule hii. Ninaahidi kwamba nitafuata sheria zote za shule na kutimiza wajibu wangu katika muda wote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Sitajihusisha na mgomo wala kuchochea mgomo, makosa ya jina au kujihusisha na vitendo vinavyoweza kuhatarisha Amani ya shule hii. Kwa jinsi hiyo, uongozi wa shule uchukue hatua ya kuniondoa au kunisimamisha masomo au adhabu yoyote pale nitakapokwenda kinyume na maagizo, kanuni na sheria za shule. Ninaahidi pia kuwa nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu.

Saini ya mwanafunzi: ……………………………………………………………………………
Jina la mwanafunzi: ……………………………………………………………………………..
Tarehe: ………………………………………………………………………………………

Saini ya mzazi au mlezi: ………………………………………………………………………
Jina la mzazi au mlezi: …………………………………………………………………………
Namba ya simu ya mzazi au mlezi: ……………………………………………………………..
Tarehe: ………………………………………………………………………………………

**TAARIFRA MUHIMU KWA MWANAFUNZI**

**1.** Jina lako ………………………………………………………… (jina hili ni lazima lifanane na jina linalosomeka kidato cha nne).

**2. BABA.**

i) Jina la baba yako: ……………………………………………………………………

ii) Yu-hai: NDIYO , ☐ HAPANA ☐ (weka alama ya vema panapostahili).

iii) Kama amefariki, taja ni lini: …………………………………………………………

iv) Kama yu-hai, anuani yake ni: ………………… namba ya simu: ……………………

v) Kazi na cheo chake: …………………………………………………………………

vi) Dini ya baba yako: …………………………………………………………………..

**3. MAMA.**

vii) Jina la mama yako: …………………………………………………………………

viii) Yu-hai: NDIYO ☐ , HAPANA ☐ (weka alama ya vema panapostahili).

ix) Kama amefariki, taja ni lini: …………………………………………………………

x) Kama yu-hai, anuani yake ni: ………………… namba ya simu: ……………………

xi) Kazi na cheo chake: …………………………………………………………………

xii) Dini ya mama yako: …………………………………………………………………

**4. MLEZI.**

i) Unaye mlezi? (mlezi ni mtu asiye mzazi wako) anayekutunza na kukuhudumia kwa chakula, malazi n.k. NDIYO , HAPANA (weka alama ya vema panapostahili).

ii) Kama ni NDIYO:

a) Jina la mlezi huyo ni: ……………………………………………………………..

b) Uhusiano wako na mlezi (mjomba, rafiki, kaka, shangazi n.k): ……………….

c) Anuani ya mlezi wako: ……………………………………………………...

d) Kazi ya mlezi wako: …………………………………………………………

e) Namba ya simu ya mlezi wako: ………………………………………………..

**5.** Jina la mtu anayepelekewa ripoti zako za shule kama si baba/mama au mlezi wako ni:

i) Jina: ………………………………………………………………………………

ii) Anuani yake: ……………………………………………………………………...

iii) Namba yake ya simu: ………………………………………………………………

**Kumbuka.**

Ambatanisha nakala zifuatazo katika fomu hii:

i) Result Slip ya mwanafunzi ya Kidato cha nne.

ii) Cheti cha mwanafunzi cha kuzaliwa.

**MFANO WA SARE ZA SHULE**

| **1** | **2** | **3** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
|  T-SHIRT YA SHULE |  SWETA LA SHULE |  SARE YA MICHEZO |
| **4** | **5** | **6** |
|  SARE YA SHULE |  SARE YA MICHEZO – TRACKER |  SHAMBA DRESS |